# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# MAHAKAMA

## TANGAZO LA KUHUISHA VYETI VYA UDALALI NA WASAMBAZA NYARAKA WA MAHAKAMA

**A. UTANGULIZI**

Mahakama ya Tanzania inapenda kuwakumbusha Madalali na Wasambaza Nyaraka wote wa Mahakama walioteuliwa kufanya kazi katika Mikoa mbalimbali Tanzania Bara kuwa Vyeti vyao vya Udalali wa Mahakama vitafikia ukomo tarehe 31 Januari, 2026 kwa mujibu wa Kanuni ya 5 (6) ya ***Kanuni za Madalali wa Mahakama na Wasambaza Nyaraka za Mahakama Na. 363 za Mwaka 2017 (The Court Brokers and Process Servers (Appointment, Remuneration and Disciplinary) Rules, GN No. 363 of 2017)***. Hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 12 ya Kanuni hizo ***(Kanuni za Madalali wa Mahakama na Wasambaza Nyaraka za Mahakama Na. 363 za Mwaka 2017 (The Court Brokers and Process Servers (Appointment, Remuneration and Disciplinary) Rules, GN No. 363 of 2017),*** Kamati ya Uteuzi na Nidhamu ya Madalali wa Mahakama na Wasambaza Nyaraka za Mahakama pamoja na majukumu mengine, imepewa jukumu la kuhuisha Vyeti vya Madalali wa Mahakama. Kwa kuzingatia Kanuni tajwa hapo juu Madalali wote wa Mahakama wanapaswa kuhuisha Vyeti vyao katika kipindi cha miezi mitatu (3) kabla ya kufikia ukomo wake.

## B. SIFA ZA DALALI WA MAHAKAMA

***Kamati ya Uteuzi na Nidhamu ya Madalali wa Mahakama na Wasambaza Nyaraka za Mahakama*** haitahuisha Cheti cha Dalali wa Mahakama endapo atakuwa ameshindwa kukidhi vigezo vilivyowekwa na Kanuni ili kuhuisha Cheti cha Udalali wa Mahakama na pia ikithibitika kuwa amekiuka taratibu na maadili ya utendaji kazi ya Udalali wa Mahakama na kukutwa na sifa kama zilivyoainishwa katika Kanuni ya 13 (1) ya ***Kanuni za Madalali wa Mahakama na Wasambaza Nyaraka za Mahakama Na. 363 za Mwaka 2017 (The Court Brokers and Process Servers (Appointment, Remuneration and Disciplinary) Rules, GN No. 363 of 2017).***

## C. NAMNA YA KUFANYA MAOMBI

Barua zote za maombi ya kuhuisha Vyeti vya Udalali wa Mahakama zitumwe kwa Katibu wa ***Kamati ya Uteuzi na Nidhamu ya Madalali wa Mahakama na Wasambaza Nyaraka za Mahakama*** ambaye ni Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania kupitia kwa Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi (Mkoa) ambapo anapofanyia kazi. Aidha, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi (Mkoa) ana wajibu wa kukagua ofisi, ghala na yadi ya Mwombaji na kuandaa taarifa ya siri ya kazi ya Udalali wa Mahakama itakayoainisha; pamoja na mambo mengine utendaji, uwezo, nidhamu, maadili na mwenendo wa Dalali wa Mahakama na kuiwasilisha kwa Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania.

## D. BARUA YA MAOMBI YA KUHUISHA CHETI CHA UDALALI WA MAHAKAMA IAMBATISHWE NA: -

(i) Kivuli cha Cheti cha Dalali wa Mahakama kinachoisha muda wake.

**(ii)** Ufupisho wa taarifa za mwombaji (CV). ***(Taarifa isiwe na "Referees" ambaye ni ndugu, jamaa au rafiki mwenye uhusiano wa karibu na mwombaji).***

(iii) Kivuli cha Cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha Uraia.

(iv) Picha mbili za rangi ***(Passport size)*** zilizopigwa hivi karibuni.

(v) Fomu ya Maombi ya Udalali (Fomu Na. 6) iliyojazwa kikamilifu.

(vi) Fomu ya Wadhamini wawili wa Muombaji (Fomu Na. 5) yenye jumla ya kiwango cha udhamini kisichopungua Milioni mia nne (400,000,000/=) *(**Fomu ibandikwe picha za Wadhamini**).*

(vii) Leseni ya Biashara kutoka katika Halmashauri ya Jiji, Mji au Manispaa.

(viii) Barua ya utambulisho juu ya tabia ya Mwombaji kutoka kwa watu wanaoaminiwa. ***(Barua isiandikwe na ndugu, jamaa au rafiki mwenye uhusiano wa karibu na mwombaji).***

(ix) Nakala ya hati ya Bima ya moto, majanga na wizi ambayo ni hai kwa mujibu wa Sheria.

(x) Nakala ya Cheti cha usajili wa Kampuni ambayo Mwombaji ataitumia katika kazi ya Udalali wa Mahakama au Leseni ya Udalali wa Kawaida ***(Auctioneers' General License).***

**(xi)** ***MEMART (Memorandum and Articles of Association)*** ya Kampuni itakayotumika katika kazi ya Udalali.

**(xii)** Nakala ya uthibitisho wa malipo ya Kodi ***(TIN).***

(xiii) Taarifa ya Benki ya miezi kumi na miwili (12) ya hivi karibuni inayoonesha uwezo wa Kifedha wa Kampuni itakayotumika au uwezo wa Mwombaji.

(xiv) Hati ya kubadilisha jina ***(Deed Poll)*** iwapo kuna tofauti ya majina katika nyaraka zitakazotumika katika maombi ya Mwombaji.

(xv) Uthibitisho wa umiliki wa Ofisi, yadi na ghala la kuhifadhia bidhaa au mkataba wa upangishaji.

## E. WASAMBAZA NYARAKA WA MAHAKAMA

**BARUA YA MAOMBI YA KUHUISHA CHETI CHA WASAMBAZA NYARAKA WA MAHAKAMA IAMBATISHWE NA: -**

i. Kivuli cha Cheti cha Wasambaza Nyaraka wa Mahakama kinachoisha muda wake.

ii. Ufupisho wa taarifa za mwombaji (CV). ***(Taarifa isiwe na "Referees" ambaye ni ndugu, jamaa au rafiki mwenye uhusiano wa karibu na mwombaji).***

iii. Kivuli cha Cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha Uraia.

iv. Picha mbili za rangi ***(Passport size)*** zilizopigwa hivi karibuni.

v. Fomu ya Maombi ya Wasambaza Nyaraka (Fomu Na.7) iliyojazwa kikamilifu.

vi. Fomu ya Wadhamini wawili wa Muombaji (Fomu Na. 5) yenye jumla ya kiwango cha udhamini kisichopungua Milioni mia nne (400,000,000/=).

vii. Leseni ya Biashara kutoka katika Halmashauri ya Jiji, Mji au Manispaa.

viii. Barua ya utambulisho juu ya tabia ya Mwombaji kutoka kwa watu wanaoaminiwa. ***(Barua isiandikwe na ndugu, jamaa au rafiki mwenye uhusiano wa karibu na mwombaji).***

ix. Nakala ya uthibitisho wa malipo ya Kodi ***(TIN).***

x. Hati ya kubadilisha jina ***(Deed Poll)*** iwapo kuna tofauti ya majina katika nyaraka zitakazotumika katika maombi ya mwombaji.

## F. MAELEZO MUHIMU

Fomu zote za maombi ya kuhuisha Vyeti vya Udalali wa Mahakama na Wadhamini wake zinapatikana katika Ofisi zote za Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi (Mkoa) Tanzania Bara na Ofisi ya Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, **DODOMA**.

Kabla ya kuwasilisha maombi kwa ***Kamati ya Uteuzi na Nidhamu ya Madalali wa Mahakama na Wasambaza Nyaraka za Mahakama*** atatoa orodha ya Madalali wote wa Mahakama walioomba kuhuisha Vyeti vyao katika *Magazeti* yanayosomwa kwa wingi nchini na katika *tovuti* ya Mahakama (www.judiciary.go.tz) ili kupata maoni kutoka kwa wateja, wadau na wananchi kwa ujumla juu ya utendaji, uwezo, nidhamu, maadili na mwenendo wa Dalali wa Mahakama. Maoni yatapaswa kutumwa kupitia *barua pepe* (hcmainregistrydsm@judiciary.go.tz) au kwa anuani ya Posta ya Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania tajwa hapa chini.


Mwombaji wa kuhuisha Cheti cha Udalali wa Mahakama atakayefanikiwa kuhuisha Cheti chake atapaswa kulipa ada ya kiasi cha Shilingi laki mbili (Tsh. 200,000/=) ikiwa ni gharama ya malipo ya Cheti cha Udalali wa Mahakama.

Mwisho wa kupokea maombi ya kuhuisha Cheti cha Udalali wa Mahakama ni tarehe 9/01/2026 saa 9:30 alasiri.

Mwombaji wa kuhuisha Cheti cha Udalali wa Mahakama anapaswa kuandaa nakala tatu (3) na kutuma maombi yake kwa njia ya Posta ***(E.M.S)*** au kwa Mkono na kuwasilishwa kwa,

Msajili Mahakama Kuu ya Tanzania,
2 Mtaa wa Mahakama,
S.L.P 2757,
**Tambukareli 40491 DODOMA.**

Imetolewa leo tarehe 7 Novemba, 2025 na: -



E. D. Massawe

**Kny: MSAJILI**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**